

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**



PRESS RELEASE

**MAELEZO YA KATIBU MKUU WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA
WATOTO KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO
WA AFRIKA YATAKAYOFANYIKA TAREHE 16 JUNI, 2012**

UTANGULIZI:

Mwaka 1990, uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) ulipitisha Azimio la nchi 51 wanachama wa Umoja huo, kukumbuka watoto wa kitongoji cha Soweto kilichopo Afrika ya Kusini ambao waliuawa kinyama na iliyokuwa Serikali ya Makaburu ya nchi hiyo tarehe 16 Juni, 1976. Watoto hao walikuwa wakidai haki ya kutobaguliwa pamoja na haki nyingine za kibinadamu.

MADHUMUNI:

Pamoja na kukumbuka mauaji hayo ya kinyama, madhumuni mengine ya kuadhimisha siku hii ni kuwa na fursa ya kuisitiza wajibu wa Serikali za Afrika kwa watoto; kuziwezesha Serikali hizo kuandaa na kutekeleza mipango ya taifa ya kuwaendeleza watoto na kuinua kiwango cha uelewa na ufahamu wa matatizo yanayowakabili watoto wa Afrika.

Tanzania ikiwa ni nchi mojawapo mwanachama wa Umoja wa Afrika, imekuwa ikishiriki kikamilifu katika kuadhimisha siku hii kwa miaka ishirini na moja (21) mfululizo, tangu mwaka 1991.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania imekuwa ikitumia siku hii kutafakari kwa kina matatizo yanayowakabili watoto na vile vile kutafuta namna ya kuyapatia ufumbuzi

matatizo hayo. Serikali inapata pia wakati mzuri wa kutangaza sera, programu na mipango mbalimbali inayohusu masuala ya watoto na kuhamasisha jamii kuchangia kuondoa matatizo ya watoto nchini.

Kwa upande mwingine, maadhimisho haya ni sehemu ya utekelezaji wa sera zetu zinazohusu kuwaendeleza watoto, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu haki na ustawi wa watoto.

KAULI MBIU:

Kaulimbiu ya mwaka 2012 inasema “**Haki za Watoto Wenye Ulemavu: Ni Wajibu Wetu Kuzilinda, Kuziheshimu, Kuziendeleza na Kuzitimiza (The Rights of Children With Disabilities: The Duty to Protect, Respect, Promote and Fulfill)**”. Kaulimbiu hii inatukumbusha kuwa tuna jukumu la kuangalia upya utoaji wa haki za msingi kwa watoto wenye ulemavu na hasa katika miundo mbinu na utoaji wa huduma za msingi mfano elimu, matibabu n.k

SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA:

Maadhimisho haya huambatana na shughuli mbalimbali za maendeleo ambazo hufanyika kitaifa na kimkoa. Mwaka huu hapatakuwepo na maadhimisho kitaifa, bali kila mkoa utapata fursa ya kupanga namna ya kuadhimisha siku hii kulingana na rasilimali zilizopo mkoani, wilayani na vijijini.

MWISHO:

Ni matarajio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuwa vyombo vya habari vitatoa ushirikiano wa hali ya juu katika kuhamasisha jamii yetu juu ya umuhimu wa siku hii.

Vile vile, Wizara inapenda kutumia fursa hii kuikumbusha mikoa kuhakikisha kuwa siku hiyo inaadhimishwa katika maeneo yao na kwa kutumia rasilimali walizo nazo.

Mwisho, ninapenda kuchukua tena fursa hii kuwakumbusha Watanzania wote na viongozi wetu hapa nchini kuwa tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wote wanapewa haki zao za msingi pasipo kujali rangi, dini, jinsi, ulemavu na hata kabila.

Nawatakia kila la kheri katika kufanikisha maadhimisho haya.

WATOTO NI TAIFA LA LEO NA KESHO.

Kijakazi R. Mtengwa
KATIBU MKUU